

**MAKAO MAKUU**

Ghorofa ya 4, Jengo la PSSSF, Barabara ya Makole  
S.L.P. 2857, Dodoma, Tanzania

Simu: +255-26 2329002-3; Nukushi: +255-26 2329005

Barua pepe: [info@ewura.go.tz](mailto:info@ewura.go.tz)

Tovuti: <http://www.ewura.go.tz>

## TANGAZO KWA UMMA

### MWITO WA MAONI YA WADAU KUHUSU MAOMBI YA MAREKEBISHO YA BEI ZA MAJI KUTOKA MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA YA NZEGA (NZEGA WSSA) KWA MWAKA 2020/21 – 2022/23

Mnamo tarehe 20 Februari 2020 Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ilipokea maombi kutoka Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira ya Nzega (Nzega WSSA) ya kutaka kurekebisha bei za huduma zake za maji safi na usafi wa mazingira kwa mwaka 2020/21 hadi 2022/23. Majedwali namba 1 hadi 3 hapa chini yanaonesha bei na tozo za sasa na bei zinazopendekezwa.

#### Jedwali Na 1: Bei ya Sasa na Zinazopendekezwa kwa Wateja Wenye Dira (Shilingi kwa Uniti moja ya ujazo)

Kundi la Wateja	Bei ya Sasa	Maba diliko	Bei Zinazopendekezwa						
	2019/20		Jan20-Jun20	Mab adiliko	2020/21	Maba diliko	2021/22	Maba diliko	2022/23
Majumbani	1240	19%	1474	26%	1851	25%	2311	20%	2768
Taasisi	1375	19%	1635	26%	2053	25%	2563	20%	3070
Biashara	1485	19%	1765	26%	2217	25%	2768	20%	3315
Viwanda	1485	19%	1765	26%	2217	25%	2768	20%	3315
Magati	1000	19%	1189	26%	1493	25%	1864	20%	2233

#### Jedwali Na 2: Ada za Sasa na Zinazopendekezwa za Maunganisho Mapya ya Maji (Shilingi/ Maunganisho)

Kundi la Wateja	Ada ya Sasa	Ada Inayopendekezwa		
	2018/19	2019/20	2020/21	2021/22
Majumbani	Asilimia 20 ya Gharama za Vifaa vya Maunganisho	Asilimia 20 ya Gharama za Vifaa vya Maunganisho		
Taasisi				
Biashara				
Viwanda				

#### Jedwali Na 3: Ada ya Sasa na Zinazopendekezwa za Kurejeshwa Huduma ya Maji (Shilingi/Marejesho)

Kundi la Wateja	Ada ya Sasa	Ada Zinazopendekezwa					
	2019/20	Mabadiliko	2020/21	Mabadiliko	2021/22	Mabadiliko	2022/23
Majumbani	15,000	33%	20,000	0%	20,000	0%	20,000
Taasisi	16,000	31%	21,000	0%	21,000	0%	21,000
Biashara	16,000	31%	21,000	0%	21,000	0%	21,000
Viwanda	16000	31%	21,000	0%	21,000	0%	21,000

Kwa mujibu wa Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Nzega mabadiliko ya bei yataiwezesha Mamlaka kulipa gharama za uendeshaji na matengenezo katika utekelezaji wa mradi mpya wa maji wa Ziwa Victoria unaotarajiwa kuanza mwezi Machi 2020.

Kwa mujibu wa kifungu Na. 19 (2) (b) cha Sheria Na. 414, EWURA inakaribisha maoni ya wadau wote kuhusu maombi ya Mamlaka ya Maji Tabora. Wadau wanaopenda kutoa maoni wawasilishe maoni yao kwa njia ya barua pepe kwa anuani ya [info@ewura.go.tz](mailto:info@ewura.go.tz) wakati wowote tangu tarehe ya tangazo hili. Maoni kwa njia ya ujumbe wa maandishi au sauti kupitia mtandao wa WhatsApp na ujumbe wa simu ya mkononi yatapokelewa kupitia namba **+255767610599** kuanzia tarehe 16 Aprili 2020. Aidha, tarehe hiyohiyo, masanduku ya maoni yatawekwa katika ofisi za Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Nzega na Halmashauri ya Mji wa Nzega. Mwisho wa kuwasilisha maoni itakuwa tarehe 27 Aprili 2020.

Maelezo zaidi yanaweza kupatikana katika ofisi za **EWURA KANDA YA KATI, GHOROFA YA TANO, JENGO LA PSSSF; BARABARA YA MAKOLE, DODOMA** au **OFISI ZA MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA NZEGA.**

**Imetolewa na:  
MKURUGENZI MKUU**